BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Sita – Tarehe 21 Februari, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2023/2024.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

150. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kutokana na mabadiliko ya tabianchi, ripoti za kitaalamu zinaonyesha kuwa visiwa vingi viko hatarini kutoweka kutokana na ongezeko la kiwango cha maji baharini. Kuna juhudi nyingi zinazofanywa na taasisi za ndani na kimataifa katika kupambana na athari hizi, ikiwa ni pamoja na kuandaa mikutano na makongamano kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Licha ya jitihada hizi, athari za tabianchi kwa Zanzibar zinaonekana kuongezeka kila siku.

(a) Je, Serikali imewahi kufanya tathmini ya kina ya kitaalamu kuhusu athari hizi kwa visiwa vyetu kwa

upande wa mazingira, kijamii, na kiuchumi.

(b) Je, Serikali ina mikakati gani endelevu ya kukabiliana na athari hizi katika visiwa vyetu, hususan kwa kuzingatia ongezeko la shughuli za kibinadamu zinazoathiri mazingira yetu.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

44. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni jambo jema kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) limekusudia kuimarisha mpango wake wa kukuza uchumi wa kilimo nchini. Hata hivyo, katika Kambi ya JKU Msaani (Pandani) kuna uvamizi usio na mpangilio dhidi ya mashamba ya wananchi pamoja na wananchi kunyang'anywa mashamba yao ya asili yaliyo mbali kabisa na mipaka ya JKU.

(a) Je, ni lini Serikali itawashirikisha wananchi katika kutatua mgogoro huu wa uvamizi wa mashamba yao ya asili.

(b) Kwa kuwa maeneo ya JKU Msaani yanakuwa mwaka hadi mwaka bila utaratibu maalum, je, ni ipi ilikuwa mipaka ya JKU Msaani ya mwaka 1992 ukilinganisha na mipaka ya 2023 pamoja na maeneo yake ya mita za mraba.

(c) Je, utaratibu wa kulipatia hati eneo la JKU Msaani umefikia wapi.

<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

113. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Nampongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kitendo chake cha kutoa mikopo kwa wananchi bila ya marejesho yoyote ya riba kwa dhamira ya kuwawezesha wananchi hao kiuchumi.

(a) Je, ni asilimia ngapi ya mikopo hiyo imetolewa kwa wananchi.

(b) Ni kwa kiasi gani mikopo hiyo imewanufaisha na kuwakomboa wananchi kiuchumi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

56. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na kwamba uamuzi wa Serikali wa kutaka kulipa amana za wateja wa iliyokuwa Benki ya FBME Tawi la Zanzibar unaweza kuwa na manufaa ya kiuchumi, bado wadau wengi wanalalamikia usiri na utaratibu unaotumiwa na Serikali katika kulitatua jambo hili.

(a) Je, ni ipi dhima ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) katika kulipa amana za iliyokuwa Benki ya FBME Zanzibar.

(b) Je, ni kwa mkataba upi kati ya FBME na SMZ unaoilazimisha SMZ kulipa amana za waathirika wa iliyokuwa Benki ya FBME Zanzibar.

(c) Je, ni kwa vipi SMZ imeweza kurejesha fedha walizowalipa waathirika wa ‘Master Life’ na kwa vipi itaweza kuzirejesha fedha watakazowalipa waathirika wa FBME.

115. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kiasi gani Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imeweza kuboresha na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kwa namna gani imeweza kuleta matokeo chanya nchini

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

88. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali yetu kwa kujali elimu kwa wananchi wake na kwa muda mrefu sasa imekuwa inasafirisha wanafunzi mbali mbali nje ya nchi na kuwalipia gharama za masomo au kuratibu kumudu gharama hizo kupitia wafadhili mbali mbali. Hata hivyo, kuna taasisi mbali mbali binafsi, zinazowasafirisha wanafunzi hao nje ya nchi.

Ni taasisi gani za kielimu zinazobeba dhamana ya kuwasafirisha wanafunzi nje ya nchi na kwa kiasi gani zinaisaidia Serikali.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

37. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kumekuwa na utatanishi wa kauli za Serikali kuhusiana na ruhusa ya wanaume kusuka nywele ambayo inaonekana haiko sawa baina ya Wazanzibari na Wageni, wakati ilitakiwa iwe sawa kwa wote.

(a) Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na wanaume kusuka nywele ndani ya visiwa vya Zanzibar.

(b) Je, ni lipi lengo makhsusi la Serikali kukataza usukaji wa nywele kwa wanaume ndani ya Zanzibar.

(c) Je, jukumu la msingi la kulinda mila, silka na maadili ya Zanzibar ni la Serikali au wageni wanaoitembelea Zanzibar.

102. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Je, Wizara yako imechukua mikakati gani ya kuwainua wasanii wa tasnia za tamthilia na maigizo.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

27. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Pamoja na haja ya Serikali kuuza baadhi ya mali zilizochokaa, kuuzwa kwa matrekta ya kulimia kunahitaji maangalizo ya ziada.

(a) Kwa nini Serikali haioni haja ya kutoyauza matrekta hasa kwa umuhimu, uadimu na ughali wa ‘spares’ zake.

(b) Kwa nini Serikali haioni kuwa kuyaweka matrekta yaliyochakaa kutasaidia sana kuwepo kwa ‘spares’ za kutosha na za uhakika zitakazosaidia kuyahuisha mengine ambayo yapo shambani.

**Wizara ya Afya:**

5. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya.

   Utaratibu wa kutoa maiti wodini katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kutumia vitanda maalum vya maringi. Hata hivyo, vifaa hivyo vinakosa ufanisi kwa kuwa njia za sakafu za Hospitali zimechakaa na nyengine ni mbovu.

   Je, kuna mpango gani wa kuzifanyia ukarabati mkubwa sakafu hizo ili vifaa vinavyotumika kupelekea maiti monchwari vifanye kazi bila ya usumbufu.

74. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

   Kumekuwa na changamoto ya Bima ya Afya kwa wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanaoishi Dar-es-Salaam, ikiwa ni pamoja na wanaofanya kazi katika Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

   (a) Je, kwa kiasi gani Wizara yako inaifahamu changamoto hiyo.

   (b) Je, ni lini changamoto hiyo itapatiwa ufumbuzi.

   (c) Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wafanyakazi hao.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

15. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

   Kwa kuwa baadhi ya maeneo katika jimbo la Wawi kama vile Gombani, Mgogoni, Mkoroshoni na kadhalika yanakabiliwa na changamoto ya kutopata maji ya uhakika, na kwa kuwa huduma ya maji ni miongoni mwa huduma ya msingi katika maisha ya mwananchi.

   Je, ni lini wananchi wote wa jimbo la Wawi watapata huduma ya maji ya uhakika.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

10. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Je, lini Serikali itahakikisha mfumo wa uuzaji zao la mwani una wanufaisha wakulima badala ya wafanyabiashara wachache.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

58. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo jema kwamba nchi yetu imekuwa na ujenzi wa barabara katika sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba. Hata hivyo, utaratibu ulio rasmi na wa uhakika wa tathmini ya rasilimali na ulipaji wa fidia ni miongoni mwa kero kwa wananchi kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, ni upi utaratibu wa kuyafidia majengo na rasilimali za Serikali katika mchakato wa kupisha ujenzi wa barabara.

(b) Je, ni upi utaratibu wa kusamehe fidia za nyumba na rasilimali nyengine wakati wa kupisha ujenzi wa barabara.

(c) Je, kwa miaka mitatu iliyopita (2020/2021 – 2022/2023), ni wananchi wangapi na kiasi gani cha fedha wamesamehe malipo ya fidia kwa ajili ya kupisha shughuli za maendeleo zikiwemo shughuli za ujenzi wa barabara.

121. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa na nia ya kujenga uwanja wa Kitogani na Mwambe, lakini mpaka sasa kwa upande wa Kitogani na Mwambe hakuna hatua yoyote ya ujenzi inayoendelea.

(a) Je, ile azma ya Serikali bado ipo katika kuvitengeneza viwanja hivyo.

(b) Ni lini kazi ya ujenzi huo itaanza.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**21 Februari, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**